

**UCHANGANUZI LINGANISHI WA MALEZI YA WATOTO KATIKA MICHEZO YA KUIGIZA YA
KIGEZI UNIVERSAL ACTORS NA YA JAMII HALISI**

1 Karuhanga Deusdedit, 2 Dr Beverlyne Asiko Ambuyo PhD

1, 2 Metropolitan International University

IKISIRI

Katika tasnifu hii mtafiti ameonyesha malezi ya watoto na jinsi yanavyoshughulikiwa na wahusika katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors ambayo ina mkusanyiko wa michezo ya kuigiza ya wahusika mbalimbali ambao ni wa kabila ya kikiga. Michezo hii imechangia pakubwa katika malezi ya watoto katika jamii ya Wanyankore. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni ambayo ni: Kubainisha na kuchanganua vipengele mbalimbali vya kimtindo ambavyo vimetumika katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors, Kuchunguza maudhui yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors, Kutathmini dhima ya michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors katika malezi bora ya watoto na jamii halisi. Utafiti huu umeonyesha kwamba watoto wana changamoto nyingi katika jamii ambazo ni lazima hatua ya dharura ichukuliwe ili kuokoa kizazi kijacho. Mtafiti ameshughulikia michezo mitano ya kuigiza ambayo alichaguliwa kwa kutumia sampuli lengwa, pia alikusanya data kwa kutumia mbinu ya utazamaji, mahojiano, hojaji na upitiaji wa nyaraka na data ilichanganuliwa kwa mbinu ya maelezo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uamilifu. Kwa mujibu wa Wallace na Wolf (1980), nadharia ya Uamilifu iliasisiwa na wanasosholojia Auguste Comte (1787-1857), Harbert Spencer (1830-1903), Vilfredo (1848-1923) na Emile Durkheim (1858-1917). Nadharia ya Uamilifu huzingatia kuwa fasihi simulizi ina utenda kazi katika mfumo wa jamii iliopo. Beja (2000) anafafanua kuwa Uamilifu ni kazi ambapo kitu hufanya katika mfumo wa jamii ambamo kitu hicho kimo. Dhana hii ni sahihi kwani tanzu na vipera vya fasihi simulizi ikiwemo michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*, hutegemea moja kwa moja uhusiano na michezo ya kuigiza ya utanzu au kipera hicho na jamii husika. Kwa hivyo, mwanafasihi hujihusisha na usanifu wa kazi fulani ya fasihi kwa mujibu wa utendakazi wake katika jamii. Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi simulizi ina jukumu la kukidhi matakwa ya jamii kulingana na tabia na kaida za wanajamii. Dhana ya michezo ya kuigiza ya fasihi huonesha dhima zinazotekelezwa na utamaduni au tanzu na vipera

vya fasihi simulizi kulingana na muelekeo wa jamii husika. Baada ya kufanya utafiti huu kwa kina, mtafiti aligundua kwamba ni kweli watoto katika jamii tofauti huwa na changamoto sawa kama vile kujiunga na vikundi vya vijana wenye uonzo wa maadili na tabia nyingine mbovu kama kuvuta sigara uwizi na ukahaba. Utafiti huu utakuwa wa muhimu katika uwanja wa fasihi kwa sababu utawatia hamu watafiti wa baadaye kutaka kuvumbua masuala yanayozingatiwa katika malezi ya watoto katika ya kuigiza mingineyo.

Utangulizi

Kigezi Universal Actors ni kundi ambalo lilianzishwa na Bw. Abrahamu Rukanga katika mwaka wa 1980. Lengo kuu la kundi hili hadi leo ni kuburudisha na kuhamasisha jamii kuhusu mambo mbalimbali haswa mambo ya familia na utunzaji bora wa watoto. Hapo mwanzoni, kundi hili lilikuwa likiitwa "Kinimba" baadaye likabadilishwa na kuitwa *Kigezi Universal Actors* katika mwaka wa 2000 ambapo lilikuwa kundi mashuhuri la kuburudisha na Kuigiza hasa visa kuhusu utunzaji bora wa watoto. Baadhi ya michezo ya kuigiza waliyoanza nayo ni kama vile; *Tindarwesire*, *Baryanengwe na Omwaana w'abandi*. Kundi hili linapatikana katika mkoa wa Magharibi wilayani Kabale nchini Uganda. Mbali na Abrahamu Rukanga, waasisi wengine ni kama vile Elias Rutamirika, Sunday Sam na Elisha Rukanga. Michezo hii ya kuigiza imeenea na kusambaa kote katika mkoa wa Magharibi na mikoa jilani kama vile sehemu za Lyantonde na Masaka katika mkoa wa Uganda-kati. Michezo hii imechagua pakubwa katika kuhamasisha jamii kuhusu uzingativu wa tabia mwafaka katika jamii. Kama lengo lao kuu, *Kigezi Universal Actors* wamezidi kutunga michezo ya kuigiza kama: *Kamuhagama, omuntu w'eishokye, Akamigano ka rukundo, Buri mbuzi aha nkondo yayo n'Orweshigikyire*. Michezo hii inajumulisha masuala ambayo hulenga jamii ya kisasa hasahasa maisha ya watoto. Jamii ya kisasa ina vijana ambao wana uozo wa maadili kama vile kututa sigara, kuiba, ukahaba, kutoheshimu wanaowazidi umri, kukataa kufanya kazi za nyumbani nakhadhalika. Kundi hili la *Kigezi Universal Actors* lina michezo ya kuigiza yenye kushughulikia masuala mapana katika maisha ya mwanadamu. Kuna michezo ya

kuigiza kuhusu mazingira, unafiki, ufisadi, ubinafsi, mapenzi, ndoa, utaifa, msako wa nafsi, ulemavu, mauti, falsafa kuhusu maisha, nasaha, maadili, malezi na kadhalika. Kwa hiyo, huenda michezo ya kuigiza ina uwezo wa kuwaonya, kuwaelimisha, kuwatahadhalisha, kuwaelekeza na kuwakosoa katika ujumbe uliomo kwenye michezo hiyo.

Usuli wa Utafiti.

Suala la malezi ya watoto limekuwa likisisitizwa katika Nyanja tofautitofauti hasa kisiasa na kijamii. Kisiasa, viongozi wamekuwa wakijali malezi na maisha ya watoto na hii ndiyo sababu kunakuwa na afisa kwa kamati za vijiji anayeshughulika na masuala ya watoto. Kijamii, kila familia ina wajibu wa kuadilisha watoto. Hali ya malezi ya watoto pia imekuwa ikisisitizwa katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors ambapo wahusika wana na visa vinavyobeba vipengere vya watoto. Jamii mbalimbali zina kwa muda mrefu zimejaribu kutibu watoto wao kimaadili kwa ajiri ya kujenga vizazi vyenye manufa kwa jamii, sio majambazi ambao hupingamiza maendeleo na mwelekeo wa jamii.

BAKIZA (2010) wamelifasili neno hilo kwa kusema kuwa mtoto ni “Mtu mwenye umri kuanzia siku moja hadi miaka kumi na nane au mtu aliye chini ya umri wa wazazi wake”. Bakize (2014), amemuangalia mtoto katika mikabala tofauti kutegemea na mwege wa mtoa maana. Anaeleza kuwa dhana ya neno mtoto ina utata na hufahamika kwa uwazi kutokana na mahali ilipotumika. Ametoa maana ya neno hilo kidini, kijamii, na kiasasi kama ifuatavyo: Kidini neno mtoto hutumika kama ni watumishi wa Muumba, huaminika kuwa watu wote ni watoto wa Mungu, kwa hivyo, hata kama watakuwa ni watu wazima bado watabaki kuwa ni watoto. Kijamii ni kuwa mtu anapozaliwa anakuwa ni mtoto mbele ya wazazi wake. Atabaki na sifa hiyo ya utoto mbele wazazi wake hata kama atakuwa na umri mkubwa na kuwa na mvi kama walivyo wazazi wake. Mamlaka za serikali, asasi na mashirika ya kitaifa na kimataifa

kama vile, shirika la kazi duniani (ILO) yanatambua kuwa mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane. Bakize anahitimisha kwa kusema kuwa mtoto ni mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane, aliye na fikra changa kutokana na umri wake, ambaye yupo chini ya uangalizi wa watu wazima kimalezi, kimahitaji na asiye na uhuru wa kujitawala kimatendo. Katika utafiti huu, watoto waliokusudiwa ni wale wenye umri chini ya miaka kumi na tatu ambao ndio wanaojishughulisha zaidi na michezo iliyokusudiwa.

Shima (2012) akiwanukuu wataalamu mbalimbali katika dhana ya mtoto ametoa fasili mbalimbali, miongoni mwa wataalamu hao ni; Bisht R. aliyefanya utafiti na kuwagawa watoto katika vipindi vitatu ambavyo ni; kwanza, utoto wa awali unaoanzia mara baada ya kuzaliwa hadi kufika miaka kumi hadi kumi na mbili, ambapo mtoto huwa na utambuzi mdogo na utegemezi. Pili, ni kipindi cha baleghe, hiki ni kipindi ambacho mtoto huwa amekomaa kiakili na kuweza kutofautisha kati ya jema na baya, kipindi hiki ni kati ya miaka kumi na mbili hadi kumi na mitatu. Tatu, ni kipindi cha ujana/utoto mpevu. Hiki ni kipindi cha miaka kumi na nne hadi kumi na tano, watoto wanakuwa na uelewa mkubwa ingawa bado wanakuwa chini ya uangalizi wa wazazi wao.

Pia amemnuuu Piajet kama alivyo Kigezi Universal Actorsliwa na Seefeldt A (2007) ambaye alifanya utafiti katika hatua za utambuzi wa watoto na kutaja hatua nne ambazo ni; kwanza, uchanga, kipindi cha baada ya kuzaliwa hadi miaka miwili, pili, utoto wa awali, miaka miwili hadi miaka saba, tatu, utoto wa kati, miaka saba hadi kumi na moja na nne ni baleghe, miaka kumi na moja hadi kumi na sita. Kwa jumla dhana hii ya mtoto na ukomo wake imekuwa na utata, bali, kama ilivyoelezwa kabla ni kuwa watoto wanaokusudiwa katika utafiti huu ni wale walio chini ya umri wa miaka kumi na mitatu.

Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia ya, kwa sababu nadharia ya hujikita katika ukweli wa hali halisi ya maisha katika jamii mahsusi na michezo ya kuigiza hushughulikia malezi mazito na muhimu yanayomhusu binadamu katika jamii. Michezo ya kuigiza ni utanzu wa fasihi ambao kimsingi hudhamiriwa kuigizwa mbele ya hadhira. Utendaji huu hufanywa na viumbe ambao aghalabu hutumia lugha. Viumbe hawa huiga mambo yanayopatikana na jinsi yanavyoonekana katika jamii. Lugha ya viumbe hawa kadhalika huingiliana kwa kiasi kikubwa na lugha ya jamii inayohusika. Maigizo yanapoandikwa, matokeo yake ni tamthilia. Tamthilia inapowasilishwa jukwaani na kuigizwa, inakuwa kitengo cha sanaa ya malezi ya watoto.

Michezo ya kuigiza huhusisha michezo ya kuigiza ikiwemo michezo ambayo huakisi hali halisi ya maisha ya wanajamii. Michezo hiyo huwa ni zao la jamii ingawa hufikishwa kisanii. Michezo ya kuigiza katika kazi za sanaa, husaidia uwelewa wa hadhira kwa kile kinachowasilishwa mbele yao. Tendo hilo vilevile huleta wa mambo mbalimbali ya kimaisha kama vile maonevu, dhulma au utetezi juu ya kadhia iliyopo katika uwasilishaji wenyewe. Katika malezi ya watoto hali kama vile za kuhuzunisha, kuliza, kujenga huruma au kufurahisha hujitokeza. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors kama kazi za fasihi simulizi ikiwemo ni roho ya ufaisi wa kazi yenyewe kama alivyobainisha Songoyi (1997).

Kipindi hiki cha maisha hudhihirika kuwa cha mpito, ambapo mtoto anabadilika kutoka maisha ya utoto hadi utu uzima. Data ya kufafanua uamuzi huu ilitolewa katika sehemu inayoifasili dhana ya Watoto. Nchini Uganda, kuna kauli kwamba, watoto ni viongozi wa kesho; hii ni kauli ambayo hutolewa mara kwa mara na viongozi katika majukwaa mbalimbali ya siasa ili kuwapa watoto motisha. Utafiti huu unalenga kuonyesha jinsi michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors inasawiri malezi ya watoto na wake katika jamii.

Suala la utafiti.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu malezi ya watoto Kama vile utafitoi wa Rotich (2008) na Ussi (2010), ambao wamebainisha umuhimu wa malezi bora ya watoto katika harakati zao za kimaisha, fasihi inayowahusu na kugusa maisha yao na harakati za ukuaji katika jamii. Hakuna utafiti ambao umewahi kufanywa kuhusu uchunguzi linganishi wa malezi ya watoto katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na ya jamii halisi. Uchache wa tafiti katika michezo ya kuigiza umechangia kwa kiasi kikubwa kuonyesha umuhimu wa michezo ya kuigiza kwa kuzingatia kipengere cha burudani kwa watoto sio katika kipengere cha malezi ya watoto kama tanzu la fasihi simulizi. Watafiti tangulizi pia wamechukulia na kudhani kwamba wazazi huwapa watoto wao malezi ya kutosha. Suala hili lilizusha utashi na haja ya kutaka kujua malezi ya watoto yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza hasa ya *Kigezi Universal Actors* na ya jamii halisi. Hili ndilo pengo la kitaaluma ambalo mtafiti alilenga kuziba. Baadhi ya wazazi katika jamii wafikiri kuwa watoto kuitazama michezo ya kuigiza kwenye runinga au ana kwa ana katika sherehe au jukwani huwa wanajipumbaza. Fikra hizo za wazazi zimesababisha kuwepo kwa mtazamo hasi juu ya umuhimu wa michezo ya kuigiza katika jamii. Utafiti huu ulilenga uchunguzi linganishi wa michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* katika malezi ya watoto katika jamii halisi ili kuziba pengo la kitaaluma (limeshatajwa).

Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi malezi ya watoto yanavyosawiriwa katika Michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na jamii halisi.

Malengo mahsusi ya utafiti huu yalikuwa: -

- a) Kubainisha na kuchanganua vipengele mbalimbali vya kimtindo ambavyo vimetumika katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors
- b) Kuchunguza maudhui yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors
- c) Kutathmini dhima ya michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors katika malezi bora ya watoto na jamii halisi

Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo.

- 1. Ni michezo gani ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors inayohusika na malezi ya watoto?
- 2. Kuna maudhui gani yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors?
- 3. Michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors ina dhima gani katika malezi ya watoto na jamii halisi?

Umuhimu wa Utafiti

- 1. Utafiti huu utakuwa ni miongoni mwa tafiti za awali zitakazoshughulikia Michezo ya kuigiza katika jamii halisi kwa kurejelea michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors. Kwa kuchambua matumizi ya michezo ya kuigiza teule ya Kigezi Universal Actors kutawawezesha wahakiki na watafiti kwa jumla kuvifahamu vipengele vya Michezo ya kuigiza na wake katika jamii.
- 2. Utafiti huu pia utakuwa na umuhimu kwa watafiti wa baadaye kufahamu namna Michezo ya kuigiza inavyochangia katika kukuza na kuendeleza malezi bora ya watoto katika jamii husika na kuvutiwa kutafiti zaidi namna michezo ya kuigiza unavyohusiana na vipengele vingine vya kifani katika kukuza maudhui. Si hivyo

tu, bali pia utafiti huu utahamasisha watunzi wengi zaidi kutunga michezo kwa umma kama hii ya *kigezi Universal Actors*.

3. Utafiti huu pia utakuwa rejeleo la kutumainiwa katika uchunguzi wa fani ya michezo ya kuigiza utakaokuwa ukifanywa na watafiti wa baadaye. Kutokana na utafiti huu, watafiti wa baadaye wataweza kuibua maarifa mapya ya kutafitiwa kwa lengo la kutimiza madhumuni yao ya utafiti na kuikuza zaidi taaluma ya fasihi.
4. Wasomi watafanikiwa katika usomi wao ikiwa wataelewa michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* kwa kuwa michezo ya kuigiza ni uti wa mgongo katika ufunzaji na uelewekaji wa jamii halisi. Vipengele vya michezo ya kuigiza vinapoeleweka inakuwa rahisi kuelewa dhamira na maudhui ya mwandishi kwa kuwa vinatekeleza dhima ya ujenzi wa dhamira na maudhui hayo (Njogu na Chimerah, 1999).
5. Katika utafiti huu mtafiti ataonyesha kuwa mbinu zinazomfaulisha mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake ndizo bora zaidi katika kazi ya fasihi. Hii inatokana na ukweli kuwa mbinu hizi husaidia katika kuelezea ujumbe wa mwandishi kwa mantiki. Kwa wale wanaotaka kuwa waandishi, utafiti huu utakuwa ni wa manufaa kwani utawasaidia kuelewa umuhimu wa vipengele vya michezo ya kuigiza ambavyo vitachangia ari ya kuitazama michezo hii ili wataalamu watarajiwa waweze kutunga michezo yao kwa njia bora zaidi. Pia kwa wahakiki wa fasihi, utafiti huu utawafaa katika kuandika tafiti zao kwa ubora zaidi kwani utafiti wa leo ni msingi wa ule utakaofanywa kesho.

Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uamilifu. Kwa mujibu wa Wallace na Wolf (1980), nadharia ya Uamilifu iliasisiwa na wa nasosholojia Auguste Comte (1787-1857), Harbert Spencer (1830-1903), Vilfredo (1848-1923) na Emile Durkheim (1858-1917).

Baadaye nadharia hii iliendelezwa na mwanaanthropolojia Radcliffe Brown (1881-1955) na Malinowski (1884-1942). Malinowski alizingatia fasihi simulizi kwa mujibu wa uamilifu au utenda kazi wake katika jamii. Nadharia ya Uamilifu huzingatia kuwa fasihi simulizi ina utenda kazi katika mfumo wa jamii iliopo. Beja (2000) anafafanua kuwa Uamilifu ni kazi ambapo kitu hufanya katika mfumo wa jamii ambamo kitu hicho kimo. Dhana hii ni sahihi kwani tanzu na vipera vya fasihi simulizi ikiwamo michezo ya kuigiza, hutegemea moja kwa moja uhusiano na michezo ya kuigiza ya utanzu au kipera hicho na jamii husika. Kwa hivyo, mwanafasihi hujihusisha na usanifu wa kazi fulani ya fasihi kwa mujibu wa utendakazi wake katika jamii.

Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi simulizi ina jukumu la kukidhi matakwa ya jamii kulingana na tabia na kaida za wanajamii. Dhana ya michezo ya kuigiza ya fasihi huonesha dhima zinazotekelezwa na utamaduni au tanzu na vipera vya fasihi simulizi kulingana na mwelekeo wa jamii husika. Wasomi wengine wa fasihi simulizi walioendeleza fasili hii iliyotolewa na Malinowski kuhusu nadharia ya Uamilifu ni pamoja na Okpewho, Leech na Firth.

Wasomi hawa walisisitiza kwamba kipande cha kazi cha fasihi simulizi kinapaswa kifanye kazi kwa mujibu wa mfumo wa jamii ulivyo. Kwa hivyo, vipengele vya uhusiano, matakwa, utamaduni na mfumo wa jamii, vina nafasi kubwa katika kipande cha kazi cha fasihi simulizi kinachoshughulikiwa. Fasili hii imetoa dira kuwa kazi za fasihi simulizi ikiwemo michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors, hutekeleza mahitaji au matakwa ya jamii. Kwa hivyo mihimili ifuatayo huzingatiwa katika kuitekeleza dhima hiyo.

- i. Uelezaji wa kipande cha utendaji wa fasihi simulizi kama kazi ya sanaa iliyomo katika jamii yenye jukumu linaloitikia matakwa ya wanajamii.
- ii. Uendelezaji wa kipande cha utendaji cha fasihi simulizi katika jamii.
- iii. Utendakazi wa jukumu au dhima ya kipande cha utendaji cha fasihi simulizi katika jamii.

Kwa kuwa nadharia ya Uamilifu inasaidia sana katika kuchambua dhima za kazi ya fasihi simulizi katika tanzu zake, imekuwa na umuhimu mkubwa wa kutumika katika utafiti huu. Rotich (2008) ametoa maelezo kwamba, utanzu wowote wa fasihi simulizi hutumiwa katika mazingira tofauti ili kutekeleza wajibu maalumu. Kwa kauli hiyo, ni wazi kuwa kazi za fasihi simulizi kama michezo ya kuigiza huweza kuathiriwa na mabadiliko ya wakati na mazingira, lakini uamilifu wake hutegemea mazingira na muktadha wa matumizi. Pamoja na kuwa michezo ya kuigiza haimudu kupingana na mabadiliko ya mazingira, muktadha na maisha, uamilifu wake hubakia vilevile kulingana na mahitaji na matakwa ya jamii iliopo.

Ufafanuzi uliotangulia umedhihirisha kwamba nadharia ya uamilifu ndio nadharia faafu katika kuchunguzia michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actots* katika jamii. Michezo ya kuigiza ni kipande cha utendaji kinachohusiana na fasihi simulizi, kwa hivyo, kinaweza kuchunguzwa kwa kutumia nadharia hii.

Mihimili ya nadharia ya Uamilifu iliyotumika katika kukamilisha madhu muni ya utafiti huu ni mitatu. Mhimili wa kwanza ambao ni; uelezaji wa kipande kazi cha fasihi simulizi kama kazi ya sanaa iliyomo katika jamii yenye jukumu linaloitikia matakwa ya wanajamii, ulitumika kuelezea kuwa michezo ya watoto ni kazi ya sanaa. Mhimili huu umeitikia matakwa ya jamii kwani michezo yote ilichezwa kwa mujibu wa kaida na utamaduni wa jamii husika. Mhimili wa pili ambao ni; uendelezwaji wa kipande kazi cha fasihi simulizi katika jamii, ulitumika kutathmini uundwaji wa michezo ya watoto

na uwasilishwaji wake. Maelezo ya uwasilishwaji wake yatatumika kubainisha uendelezaji wa michezo hiyo kama kipande kazi cha fasihi simulizi. Mhimili wa tatu ambao ni; utendaji wa jukumu au dhima ya kipande cha utendaji cha fasihi simulizi katika jamii, utatumika kutathmini dhima mbalimbali za Kuigiza katika michezo ya kuigiza ya Kigezi Universal Actors. Hatimaye ni kuwa nadharia hii imewezesha kubaini dhima mbalimbali zinazotekelezwa na michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na mguso wake kwa maisha ya jamii.

MBINU ZA UTAFITI

Muundo wa Utafiti

Muundo wa kimaelezo ulitumika katika kushughulikia utafiti huu ili kuafikia madhumuni yake matatu. Data mtafiti aliyochanganua itatokana na usomaji na uhakiki wa vitabu na machapisho mbalimbali vinavyohusu michezo ya kuigiza, hojaji na makuigizaliano kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti. Nadharia ya utafiti itamwezesha mtafiti kuainisha, kuchanganua na kufasiri data iliyokusanywa ili kufikia madhumuni ya utafiti huu.

Eneo la utafiti.

Utafiti huu ni nyanjani na kwa hiyo ulifanyika katika eneo la Maziba wilayani Kabale ambapo kuna wahusika wa michezo hii na vijumba vya filamu ambapo rekodi za michezo itakayoteuliwa. Sababu za kuchagua eneo hili ni upatikanaji rekodi nyengi za Michezo ya Kigezi Universal Actors na wahusika wa michezo hii ni wazawa wa eneo hili kwa hiyo mtafiti aliona heri wafikie wenyewe na kuwahoji ili kupata data inayohitajika.

Idadi Lengwa

Walengwa katika utafiti huu walikuwa hamsini ambamo kulikuwa wahusika watano wa michezo ya Kigezi Universal Actors, wazazi ishirini, wanafunzi na watoto ishirini na watano amabo wako kati ya miaka tisa na kumi na minane. Idadi hii lengwa itakayotajwa itamfanikisha pakubwa mtafiti katika kuafikia madhumuni ya utafiti huu.

Uteuzi wa Sampuli

Kothari (2004) anaeleza kuwa sampuli ni kikundi fulani cha vitu au watu kilichomo ndani ya mkusanyiko wa watu ambacho mtafiti anaamini kwamba kikundi hicho kitampatia taarifa anayohitaji kuhusu utafiti wake. Kwa sababu hiyo, mtafiti hulazimika kuteua kitu fulani au watu ambao huitwa kundi lengwa. Kwa hiyo katika utafiti huu, mtafiti alitumia wahusika watano (05) wa michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*, wazazi ishirini (20) na watoto ishirini na watano (25) walio kati ya miaka tisa hadi kumi na minane (9-18). Mtafiti alitumia sampuli ya aina tatu hizi za walengwa kwa sababu ndio waliokusudiwa kutoa data iliyofaa kuhusu mada ya utafiti huu yaani uchanganuzi linganishi wa malezi ya watoto katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na hali halisi katika jamii.

Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo ndio kwanza zitakusanywa kwa mara ya kwanza kabisa na kuwasilishwa katika ulimwengu wa taaluma (Kothari, 2008). Data hizi hukusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, hojaji, makuigizaliano ya kikundi lengwa, ushuhudiaji, ushiriki na usomaji makini. Data za msingi za utafiti huu zitakusanywa kwa kutumia mbinu ya hijaji, makuigizaliano na usaili. Pia, michezo mitano ya michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors: Omuntu w'ishokye, Akamigano ka rukundo, Buri Mbuzi aha nkondo yayo, Orweshigishire na Kamuhagama*. ilitazamwa kwa makini ili kupata data ya msingi itakayokusudiwa kulingana na mada ya utafiti

Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo zinakusanywa kutoka katika machapisho na maandiko ambayo tayari yapo katika maktaba (Yin, 2001). Data hizi hukusanywa kwa lengo la kujazilishia au kukazia maarifa yatakayopatikana kutokana na data za msingi. Wataalamu wa mbinu za utafiti huita mbinu hii kama ni ya kukusanyia data za utafiti mezani. Data za upili katika utafiti huu zitakusanywa kutoka katika maktaba za Chuo Kikuu cha Maseno, Chuo kikuu cha Metropolitan. Mtafiti atasoma kwa makini vitabu hasa vya kifasihi vinavyogusa michezo ya kuigiza na malezi ya watoto.

Mbinu za Ukusanyaji Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za utazamaji, hojaji, makuigizaliano na upitiaji wa nyaraka maktabani.

Mbinu ya Usaili

Usaili ni mbinu ya ukusanyaji wa data kwa kutumia maswali simulizi. Katika kutumia mbinu hii, mtafiti huwa na orodha ya maswali ambayo huyatumia katika kuwahoji watoa taarifa wake. Aidha, maswali mengine huibuliwa wakati wa mahojiano hayo ili kupata taarifa ambazo zitasaidia mtafiti kupata taarifa muhimu za utafiti. Katika utafiti huu, mbinu hii itatumika kuwahoji wanajamii mbalimbali yani wazazi, wahusika wa michezo na watoto ambao mtafiti anaamini waliweza kumpatia taarifa muhimu za kiutafiti kuhusu dhima ya michezo ya kuigiza kwa malezi ya watoto katika jamii halisi. Mbinu hii itachaguliwa ili kuweza kudadisi na kuona iwapo wanajamii mmoja maada ya mwingine huwa wanazingatia hali ya maisha ndani ya jamii.

Hojaji

Kothari (2004) anafafanua dhanna ya hojaji kuwa ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti huandaa maswali yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Mfano,

unalinganishaje michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na ya jamii halisi? Mbinu hii itatumiwa na mtafiti na itamsaidia kuzielewa malezi ya watoto waliyomo katika ya michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na ya jamii halisi. Kwa kutumia mbinu hiyo, mtafiti aliwapa majibu tofauti kutoka kwa wahusika wa michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*, wanajamii ambao ni wazazi na watoto. Taarifa za wahojiwa hao zitamsaidia mtafiti katika kufanya uchanganuzi wa utafiti wake.

Mahojiano

Mahojiano ni maswali anayoulizwa Mtafiti wana kuyajibu kwa mazungumzo. Mbinu hii humwezesha mtafiti kupata maoni kamili na hata hisia za mtafiti. Mtafiti ana uhuru wa kufafanua maswali na kumwelekeza mtafiti wa ili apate ujumbe unaolenga madhumuni ya utafiti. Mahojiano yanaweza kuwa ya ana kwa ana, kwenye simu au wavuti. Mtafiti anaweza kupata ujumbe wa ndani na ambao hauonekani moja kwa moja au mtafitiwa hata huandika. Katika utafiti huu mbinu hii itatumiwa kupata ujumbe na maoni ya walengwa wa utafiti na jamii kwa jumla kuhusu malezi ya watoto yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na ya jamii halisi. Data kutokana na mahojiano itamsaidia Mtafiti kueleza uchunguzi linganishi wa malezi ya watoto katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na ya jamii halisi.

Vifaa vya Ukusanyaji wa Data

TUKI (2004) wanafasili data kuwa ni taarifa au takwimu ambayo hutumiwa kuelezea au kuthibitisha hoja fulani. Vifaa vya kukusanyia data ni vifaa mbalimbali ambavyo hutumika katika kukusanya na kuhifadhi data za utafiti. Katika harakati za kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alitumia vifaa mbalimbali kama; kalamu, daftari na tarakilishi.

Daftari na Kalamu

Kothari (2004) anaeleza kuwa kalamu na daftari ni vifaa vya asili katika ukusanyaji wa data ya utafiti kwa kuziweka katika maandishi zile hoja zinazohusiana na mada ya

utafiti. Mtafiti alitumia kalamu na daftari katika mchalato wa kukusanya data kwa kuandika majibu ya wahojiwa pamoja na kukukuu kimaandishi maneno ya wahusika wakati mtafiti alipokuwa akiitazama michezo ile.

Tarakilishi

TUKI (2004) wanafasili istilahi ‘tarakilishi’ kama kifaa cha umeme au mashini ya kielektroniki ya kuhifadhi na kuchanganua taarifa zinazolingizwa, kukokotolea na kuongoza mitambo. Pia, kwa upande wa tarakilishi, ile itakayotumika ni Komputa pakatwa ambayo ni aina ya kompyuta au tarakilishi inayoweza kubebeka kwa urahisi kutoka sehemu moja hadi nyingine ambayo huweza kupakatwa. Katika utafiti huu, kompyuta pakatwa ilimsaidia mtafiti wakati wa kuandaa pendekezo la utafiti, kuhifadhi data zilizokusanywa, na kuandika ripoti ya utafiti.

Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ni kitendo cha kutolea ufafanuzi data zitakazokusanywa kwa namna ambayo inasaidia kujibu maswali ya utafiti na kutimiza madhumuni ya utafiti. Data za utafiti huu zitachambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaielezo kuhusu malezi ya watoto katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*.

Mkabala wa Kimaielezo

Utafiti unaohusiana na taaluma za fasihi mara nyingi huchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaielezo kwa sababu fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ili kuichambua lugha hiyo lazima kuwe na mkabala wa kimaielezo. Hii haina maana kuwa data za taaluma ya fasihi huwa hazichambuliwi kwa kutumia mkabala wa kimahesabu. Mkabala wa kimahesabu huweza kutumika kulingana na mada na madhumuni ya utafiti husika. Hata hivyo, katika utafiti huu data zitachambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaielezo ambapo maelezo mwafaka yatatolewa kwa kila dondoo lililowasilishwa katika sura ya nne ya tasnifu hii. Mkabala wa kimaielezo ni mbinu ya kuchambua data

za utafiti kwa mtafiti kutolea maelezo data hizo huku zikishadidiwa na maelezo kutoka katika nadharia na kazi tangulizi ya uamilifu.

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

Utangulizi

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi malezi ya watoto yanavyosawiriwa katika Michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*. Ili kutimiza lengo hili, malengo mahususi matatu yaliandaliwa ambayo yalikuwa ni: Kuchunguza michezo mbalimbali ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* inayohusika na malezi ya watoto, Kuchunguza maudhui yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*, Kutathmini dhima ya michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* katika malezi bora ya watoto katika jamii halisi. Mtafiti alichunguza michezo iliyoteuliwa kama vile; *Omuntu w'ishokye*, *Akamigano ka rukundo*, *Buri Mbuzi aha nkondo yayo*, *Orweshigishire na Kamuhagama*, alichunguza michezo hii kwa kina kwa kuangazia vile suala la malezi ya watoto linalojitokeza katika michezo hii kwa kugemea wahusika wanaojitokeza. Hivyo, sura hii ya nne ya tasnifu imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kwa kutumia malengo hayo matatu ya utafiti. Hii imesaidia kuiwezesha sura hii kutimiza lengo kuu la tasnifu hii kwa ufanisi.

Maudui yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*?

Sehemu hii inajibu swali la pili la utafiti ambalo lilikuwa: Kuna maudhui gani yanayojitokeza katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*?

Katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*, mtafiti alivumbua kwamba michezo hii (imeshatajwa) imebeba uwanja wa malezi ya watoto yanayowatia maadili mwafaka katika jamii. Kuna njia mbalimbali na mikabala tofauti inayotumiwa kuwatia malezi bora. Baadhi ya njia hizi zinadhihirika katika maudhui yaliomo ambayo ni:

Wasia/Onyo

Wahusika wote katika *Kigezi Universal Actors* wametoa wasia kwawatoto katika jamii. Wasia ni maagizo ya mtu kwa watu wengine ambayo anataka yatimizwe. Wahusika wote wameshughulikia hili suala la kutoa ushauri na mwelekeo kwa watoto katika utendaji wao kwa njia mbalimbali.

Katika mchezo “**Buri Mbuzi aha nkondo yayo**” mhusika Baniyahomire ameshughulikia suala hili la kutoa wasia kwa watoto. Katika mchezo huu, mhusika huyu anatoa ushauri kwa binti yake kuhusu mapenzi. Anamwonya dhidi ya kuleta aibu katika ndoa yake. Pia, anamwambia kwamba yeye hataki mapenzi yatakayomletea aibu. Mhusika anasema haya katika ubeti wa kwanza,

“Shallon wareeba shwenkazi waawe ebyamuhikaho, oyiguke ameisho neiwe otakeija kunshwaza nkahemuka ahakyo eki. Kandi ninyeenda omanyega ngu akarungi keguza.... mbwenu oyerwanire eihari. Kandi nakwehanangiriza ku orihika owa baro, yezirikye obwesigwa, bube engabo yaawe. Beingyi baremirwe amaaka ahabw’obwesigwa....”

“Shallon, umeona umeona bima imeyomkabiri shangazi yako, lazima macho yako yafunguke usije ukanitia aibu kijijini. Tena wapaswa kujua kuwa chema chajiuza..... kwa hiyo jichunge kabisa. Pia nakusihi wakati utakapofika kwenye ndoa, ujifunge mkanda wa kuaminika, uwe ngao yako. Wengi wamekosa ndoa kwa ukosefu wa uaminifu”.

Mama pia, anaendelea kumwambia binti yake mwenye miaka 18 (kumi na minane) anayejitayarishia ndoa kwamba mapenzi ya kweli hayafananishwi na chochote na hayawezi kukopwa kamwe. Jambo la muhimu kuhusu mapenzi ni kuwa na msimamo wa kuwa na mpenzi mmoja na kudumisha uaminifu. Kwa hivyo mwandishi

anazungumzia suala la uaminifu katika ndoa na kusema kwamba ndoa nyingi katika jamii zimevunjika kwa sababu ya ukosefu wa uaminifu.

Mhusika anasema kuwa ni vizuri mtoto kufanya uchunguzi mapema kwa jambo ambalo hana uhakika nalo ili apate mwelekeo mzuri utakao mfaa kutoka kwa wenzake na wale waliomzidi umri. Katika suala hili la wasia, wahusika wametoa ushauri kwa watoto kuhusu mambo yanayo husu malezi bora kama vile kubadilisha tabia na kuwa watu wema, kujiepusha na mitego ya maisha na n.k kwa sababu wao ni watu wa maana sana katika jamii. Kulingana na wazazi kijijini mtafiti aligundua kuwa kila familia ina wasia wake ambapo wazazi wanawambia watoto wao namna yakujichukua na yanayowasubiri mbereni kwa mfano mhojiwa mmoja alisema kuwa kwake motto wakike haruhusiwi kutoka nyumbani bila yeye kujua anakokwenda. Pia kuwa anawambia watoto wake wote anayopenda na anayochukia.

Elimu

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni na maishani. Katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* wahusika wameshughulikia suala hili la elimu kwa watoto. Kila mmoja wao angalau amezungumzia kuhusu mtoto na elimu katika jamii kwa jumla. Mhusika wa kwanza ambaye ameshughulikia suala hili ni Bitakashoborokire ambaye anasema kwamba ni wazi na kweli watoto katika jamii wamepata elimu, lakini cha kushangaza ni kwamba elimu hiyo haijawasaidia watoto hawa maishani. Hii ina maana kwamba elimu hiyo sio mwafaka kabisa au haina misingi kamili, kwa hivyo Bitakashoborokire anazungumza kuhusu ukosefu wa elimu bora kwa watoto. Katika maneno yake anasema anamshtumu Kamanzi ambaye ni mtoto wake wa pili katika uzazi:

“.... esente zangye zinakushashureire zikarohama.... Omuntu kugyenda ngu naza kushoma okahendera oshagaire abaandi. Toyine ntanisa n’abaandi baana abataragire mu matendekyero, nangwa ezinakushashureire kurinogira nkakimanya kare nkaba

ninza kuzinywamu enturire. Nosiinga noshusha nyoko. Kandi imwee baana bangye abasigara mushome kurungi kandi kumwahikye ahari “hindifazite” mushome ebibeinire omugasho kugira ngu mwaheza mutungye emirimo, mutakaaba nka Kamanzi awashomire ebiteine muringo akahendera ashagaire abagyeire kushoma....”

“..... pesa zangu nilizokulipia karo ziliharibika..... mtoto kwenda na lengo kuu la kusoma akamalizia kama alivyokuwa ameenda kuwasindikiza wengine. Hauna utofouti na watoto ambao hawakuenda shuleni, nilizokulipia shuleni kama ningalijua ningalizitumia kunywa pombe.

Wewe na mamako mnafanana. Lakini nyinyi watoto wangu ambao mmesalia, mjikaze kisabuni masomoni na mkifika kwenye “Chuo kikuu” mchague masomo ambayo ni ya muhimu ili mkimaliza msijitembeze bali mpate kazi bira shaka, msiwe kama Kamanzi aliyechagua vibaya masomo yake akamaliza amekwama.....”

Kama mtafiti amesema hapo awali ni vizuri kila mtoto apate elimu iliyo nzuri na itakayomsaidia na jamii yake maishani, hasaa kwa kupata ajira. Lakini jinsi ambavyo Bitakashoborokire anasema ni kwamba watoto katika jamii wamepata elimu lakini mambo wayatendayo ni sawa na wale ambao hawajasoma kabisa. Mhusika mwingine anayezungumzia suala la elimu ni Bahemuka. Katika maneno yake anampa ushauri Seforoza ambaye ni binti yake. Kuna mvutano kati ya mzazi na bintiye kuhusu suala la elimu. Tulivyoona hapo awali sehemu zingine za nchini Uganda kama vile Kaskazini, Magharibi na baadhi ya sehemu za Bonde la Ufa, ingawa elimu ni ya mila na desturi haziruhusu mtoto wa kike kupata elimu, badala yake wanaozwa mapema Rotich (2008).

Kwa hivyo Bahemuka anatoa picha hiyo wazi kwa kusema yale yanayopatikana katika jamii tofauti tofauti. Bwana Donozio anataka kumwoza bintiye ambaye bado yuko shuleni kama mambo yalivyokuwa wakati wa Donozio kinyume na yalivyo sasa. Hii ndio

sababu Bahemuka akaonyesha kwamba mambo yamechukua mkondo mpya tofauti na vile mambo yalivyokuwa hapo awali. Jambo la kushangaza ni kwamba msichana huyu Seforoza ana msimamo thabiti wa kukataa kuolewa maana anataka akamilishe kozi yake kwanza. Baba anamwambia kwamba msichana ambaye ni wa rika lake tayari ameolewa na imebakia yeye tu kuolewa kwa sababu ashopokea mahari kutoka kwa mtoto wa mzee Binshobire.

“Seforoza ningira nomanya emitwarize y’ekika kyeitu oku eri, mbwenu nyowe nabashwento yaawe tushaziremu ku oza omumaka. Tukurondeire omushaija orikuruga omuka nungyi ya Muzeyi Bishobire kandi ningyira nokimanya ku beine ebintu. Mwine Bishobire aine engyesho nungyi kandi aine esente... nahabwekyo okutandika n’erizooba otagaruka kuza aheishomero ahabwokuba n’ebintu babiretsire...”

“Seforoza nadhani wafahamu vyema mila na desturi za familia etu, sasa mimi na wajomba wako tumeamua uolewe. Tumekuchagulia mchumba anayetoka kwenye familia tajiri yam zee Bishobire nadhani hata wewe wajua eti ni matajiri. Mchumba wako bin Bishobire ana tabia nzuri na pesa....na kwa hiyo kuanzia leo usirudi shuleni kwa sababu hata mahari wameshayaleta....”.

Hii ina maana kwamba baba amekubali kumwoza binti yake hata kabla ya idhini yake. Lakini kwa sababu Seforoza anajua umuhimu wa elimu katika jamii na pia anaelewa haki zake kama mtoto anakasilika na kukataa katakata uamuzi wa wazazi wake ingawa wapi. Anamwambia babake kwa ujasiri na ukakamavu kwamba ni muhimu kwake, kwanza ni elimu si ndoa. Na kwa sababu hiyo yeye hayuko tayari kuacha shule ili aolewe. Hii inaonyesha kwamba mtoto huyu Seforoza anajua na kuelewa haki zake kama mtoto wa kike na kuelewa faida za kupata elimu. Mbaga (1981), anaeleza kuwa mtoto anayesikiliza wazazi wake huwa na hatima bora. Anaendelea kwa kueleza kuwa ingawa katika jamii mbalimbali kuna mila na desturi zinazokinzana na haki za

watotokama vile kuwaoza wakiwa bado wachanga au kuwaachisha shule, suala ambalo mtoto ana haki ya kushtaki mlezi au mzazi yake anayemtatiza kihaki.

Katika jamii mbalimbali nchini Uganda kama vile sehemu za Kaskazini na mashariki, jambo hili la kuwanyima haki zao watoto haswa wa kike kwa kuwaoza wangali wachanga linajitokeza sana.

Jambo hili pia, linapatikana katika jamii halisi kama mhojiwa momoja alithibitisha kuwa hakuna faida yakuelimisha mtoto wa kike kw sababu wanaharibu pesa za wazazi kwa kupachikwa mimba wakiwa baado wanasoma, nakwa hivyo ni vizuri aolewe mapema.

Malezi

Lihamba na Mbaga (1981), wanaeleza kuwa malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kufuata tabia na mwenendo unaostahili. Kama mtafiti alivyotaja hapo awali familia ni asasi muhimu sana katika malezi ya watoto. Katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* wahusika wameshughulikia suala hili la malezi ya watoto. Tulivyoona awali ni kwamba wazazi wengi wanachukua muda wao mwingi kufanya kazi mbali na nyumbani na kusahau jukumu lao la ulezi. Hii huchangia sana katika maisha ya watoto na husababisha mambo mabaya kama vile uhalifu, usherati, utumizi wa madawa ya kulevya na mimba zisizo halali. Lihamba anaeleza kuwa, kwa sababu watoto hukosa mwelekeo mwema kutoka kwa wazazi, ni kweli kwamba watoto hupata mwelekeo kutoka kwa malaika wao, wafanyakazi wa nyumbani na katika teknolojia kama vile mtandao, televisheni na hata sinema.

Katika michezo ya kuigiza ya *Kigyezi Universal Actors* mhusika ambaye ameshughulikia suala la ulezi katika jamii halisi ni Bitakashoborekire katika michezo ya kuigiza ambapo ni mhusika, anasema kwamba mzazi anampa binti yake mwelekeo mzuri kuhusu mapenzi. Anazungumza kuhusu mapenzi yaliyo ya adabu na heshima kwa hivyo

mzazi anamwambia bintiye kwamba ni lazima abadilishe tabia yake iwe nzuri ili atakapojihusisha na suala la mapenzi asiye akaathirika.

“Mwanawangye... omushaija agamba kabiri omukazi agamba rimwe, orurimi nakantu kakye konka nikabasha kushaisha beingi. Omukazi ayerinda munonga yaaba nagamba kandi ku aza kukora ekintu kyoona abanza kutekateka nokwebuuza ahar’iba nobwakuba nakimanya. Nsasira nigwe mubazi omubufumbo wayejarambya amaka nibagakutwaraho, kunda omushaija waawe okukira ebindi byoona kandi n’obuyakunyizye yebwa juba ekiniga okuntukirire ebyoburyo.... kandi obe omwesigwa aha mushaija waawe”.

“Mwanangu...mume husema mara mbili na mke husema mara moja, ulimi ni sehemu ndogo ya mwili lakini waweza kuharibu mengi. Mke hujichunga sana akiwa anazungumza na huchemsha bongo kabla ya kutenda au kufanya uamuzi wowote na kumuuliza mumewe ingawa tayari ana ujuzi. Usamehevu ndiyo dawa katika ndoa na usipotia moyo ndoa yako huvunjika, penda mume wako bora kuliko kila kitu, akikukosea jisahaurishe mapema ya nyuma na kutangamana na yaliyo chanya.... Pia uwe mwaminifu kwa mume wako”.

Mzazi huyu anabeba jukumu kama mzazi mzuri kumwelekeza kumsihi kudumisha uaminifu katika ndoa yake. Hii ni sawa na kusema kwamba ni heshima sana kuwa na mpenzi mmoja tu, sio vizuri kuwa kiruka njia. Kwa hivyo binti huyu anaelekezwa vizuri na mzazi wake kuhusu suala la mapenzi kwamba kuwa na mpenzi mmoja kuna faida nyingi kama vile kujiepusha na magonjwa ya zinaa jambo ambalo hujenga jamii imala yenye watoto wa thamani na mabadiliko chanya. Kulingana na jamii lengwa watoto wa kike wanakuzwa wakitunzwa mambo ya familia na namna ya kujichukuwa katika ndoa

Ukosefu wa Maadili

Kulingana na Jones (1972), Maadili ni kuwa na mwenendo mwema, kwa hivyo ukosefu wa maadili ni kinyume cha mwenendo mwema. Wahusika katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* wameshughulika suala la ukosefu wa maadili miongoni mwa watoto katika jamii. Hawa ni pamoja na Siriri, Bahemuka na Rutabundama. Wahusika hawa wameangalia suala hili kwa njia mbalimbali. Katika mchezo wa Kamuhagama, mhusika Siriri anasema kwamba anasa ni jambo ambalo halifai kabisa na kwa sababu hiyo watoto wanafaa kabisa kujitenga nalo. Anasema wale wote ambao waliingia katika anasa hawapo kwa sababu wote wameaga dunia kwa kupata magonjwa yanayouawa. Anasema kwamba kuwa na maadili mema huenda sambamba na kumcha Mungu.

*“Eminyeeto mwerinde okukunda ebimutahendekyeire,
mumarwe n’ebimwine ahabwokuba abayehanikyire
eheiguru barikweenda ebyeesente nyingi kuruga aha
bashaija abagaiga bakeitwa sirimu nendwara
z’obushambani” Mugire engyesho nungyi kandi mwerinde
okubeihwabeihwa ebintu byensi ebirikuhwaho juba....
mukunde ruhanga kandi niwe arije kubaha
ebimurikwetenga....”*

*“Vijana mjiepushe kupenda vya bure, kinai na kichache
mpatacho kwa sababu waliotamani vya ghali kutoka kwa
wanaume matajiri walifariki kwa ukimwi na majongwa mengine
ya zinaa”. Muwe na tabia nzuri na kujirinda, msishawishwe na
mapato ya siku moja ambayo ni upepo..... mpende Mungu
ambaye atatimiza mahitaji yenu”.*

Katika dondoo hili, mhusika anaendelea kuzungumzia suala hilo la ukosefu wa maadili kwa kusema kwamba, hakuna faida yoyote mtu apatayo kwa kujiingiza katika mambo yasiyo mazuri ila maangamizi kama vile magonjwa hasa ukimwi na mwisho kifo. Kwa hivyo anawahimiza watoto wote katika jamii kubadilisha mienendo iliyo mibaya hili iwe nzuri na ya kuvutia kwa kila mtu anayekutana naye.

Ndoa na Mapenzi

Akuako (2004), anasema kwamba ndoa ni makubaliano rasmi ya mwanamke na mwanaume kuishi pamoja kama mume na mke, na mapenzi ni hali ya kuingiwa moyoni na kuthamini mtu zaidi ya mwingine. Katika jamii nyingi nchini Uganda ndoa huheshimiwa sana, ndoa ni matokeo ya mapenzi. Katika utafiti huu mtafiti ameamua kuunganisha ndoa na mapenzi kama suala moja ambalo linawahusu Watoto ambao wamefika umri wa kuo na kuolewa katika jamii. Kama nilivyosema awali ndoa ziliheshimika katika kila jamii. Katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* wahusika wamezungumzia suala hili la ndoa na mapenzi kama suala ibuka katika jamii miongoni mwa watoto. Mhusika wa kwanza anayezungumzia suala hili ni Bitakashoborekire katika michezo miwili ambayo ni *Omuntu w'ishokye* na *Akamigano ka rukundo*. Katika mchezo wa *Omuntu w'ishokye*, mhusika huyu anawaonya watoto wa kike wabadili tabia maana mapenzi hayahitaji mambo ya kuleta aibu. Anasema kwamba mapenzi hayafananishwi na chochote maana hayakopwi na yanachohitaji ni uaminifu. Anaendelea kusema kwamba mapenzi hayataki maneno yenye kuudhi au kuchukiza au hata usumbufu. Haya yote yakiingia kwenye penzi la watu wawili basi penzi hilo halina budi kufumuka.

“Rukundo neyetanga okugumisiriza n’okwehangana, nayo ni nk’omwaana neyetaga okubembesereza”. Nikipuru okumanya omushaija waawe egabo kandi okamufaho. Nikireteera wamuza omumutima kandi aharikuba ari hoona aguma nakutekyerezaho...”

“Mapenzi yahitaji uvumilivu, ni kama mtoto mchanga huhitaji kubembelezwa”. Ni muhimu kujua mume mchumba wako akulacho na kumjari. Hili husababisha mapenzi ya dhati na popote aendapo huwa anakufikiri.....”.

Jambo lingine ambalo Bitakashoborekire anasema kuhusu mapenzi ni kwamba, katika mapenzi, mtu hafai kuwa na zaidi ya mpenzi mmoja kama mtafiti alivyosema hapo awali. Watu wengi katika jamii tunamoishi wana mazoea ya kuwa na wapenzi wengi kinyume na Bibilia takatifu na hii imechangia sana katika kuvunjika kwa ndoa nyingi sana. Kwa sababu hii mhusika anatoa ushauri kwawatoto kwamba ni jambo la busara kuwa na mpenzi mmoja ambaye. Hii ni kwa sababu kujihusisha na wapenzi zaidi ya mmoja huchangia sana kueneza magonjwa kama vile ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa. Kwa hivyo msimamo wa mhusika huyu Bitakashoborekire kwa watoto katika jamii kuhusu suala hili la ndoa na mapenzi ni kupendana kati ya watu wawili tu na kuwa waaminifu katika ndoa ndio penzi litakuwa tamu na la kufurahisha.

Matokeo kuhusu ya madhumuni ya utafiti.

Baada ya kufanya utafiti huu mtafiti aligundua kwamba ni kweli michezo ya kugiza ya *Kigezi Universal Actors* hushughulika malezi ya watoto. Pia makisio ya mtafiti kuwa wahusika wote katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* wana mwelekeo sawa na uhusiano wa karibu sana kimawazo kuhusu malezi ya watoto. Hili hinadhihirishwa kupitia maudhui ambayo yalikuwa ni: Wasia/Onyo, Elimu, Malezi, Ukosefu wa Maadili na Ndoa na Mapenzi. Pia, mtafiti aligundua kwamba michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* ilikuwa na dhima mbalimbali kwa watoto na jamii halisi. Dhima hizo zilikuwa pamoja na: Kukuza ushirikiano katika jamii, kufunza ushujaa na ustahamilivu, kutambulisha amali za jamii, kubainisha utamaduni wa jamii, kukuza vipawa vya watoto, kuelimisha juu maisha kwa ujumla, kufundisha maadili mema, kujenga afya, kuwafunza watoto tabia ya utatuzi wa matatizo, kuburudisha, kukuza stadi za kutambuana, kurithisha na kuendeleza asili ya jamii.

Hitimisho

Katika tasnifu hii mtafiti amechunguza jinsi malezi ya watoto yanavyosawiriwa katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na jamii halisi. Mtafiti ametumia nadharia ya uhalisia ambayo imemwongoza vizuri kuchunguza uhalisia wa malezi ya watoto yaliomo katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* na jamii halisi.

Ameshughulikia jinsi wahusika wa Michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* wanavyowasilisha malezi wa watoto. Kwa kiwango kikubwa katika utendaji wao, wahusika hujikita sana katika vipengele ambavyo ni mwafaka kwa jamii huku wakizingatia mila, desturi na utamaduni wa jamii husika bila kukinzana na maadili. Aidha, kwa kiwango kidogo, kuna visa ambavyo havimfai mtoto kuvitazama kama vile uvutaji bangi na kunywa pombe. Kwa ujumla michezo ya kuigiza imethibitishwa kuwa

ya maana sana katika jamii. Jamii inapaswa kuwashabiki wahusika wa michezo kama hii kwa sababu inachangia pakubwa katika maendeleo ya jamii.

Mchango wa pili ni uliojitokeza katika utafiti huu ni kuwa michezo ya *Kigezi Universal Actors* ina dhima mbalimbali katika malezi yake. Imegundulika kuwa dhima zinazojitokeza katika michezo ya *Kigezi Universal Actors* zina athari kubwa kwa maisha ya wana jamii. Michezo hiyo ni chemchemu ya malezi ya watoto kwa maisha yao ya utotoni na ya baadaye.

Mchango wa tatu uliojitokeza ni kubainisha dhana ya michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* watoto ambayo inaweza kutofautishwa na michezo mingine isiyo ya kuigiza. Tofauti hiyo imeweza kudhihirisha na kutanabahisha mchango mkubwa wa urithi wa jamii katika amali mbalimbali za maisha ya jamii. Michezo ya *Kigezi Universal Actors* ikiwa ni sehemu moja ya urithi wa jamii, imejitokeza kuwa ni kipengele muhimu cha kukuza, kudumisha na kuendeleza utamaduni wa jamii. Ingawa utafiti huu umefanikiwa kukamilika na kufanikiwa kulibainisha suala la malezi katika michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*, bado kuna kazi kubwa ambayo inahitajika ifanyike kwa lengo la kuiweka hai na kuendeleza michezo ya kuigiza. Kuna baadhi ya changamoto ambazo zilibainika kupitia mchakato wa kukamilisha tasnifu hii. Moja miongoni ya changamoto hizo ni kupotea kwa baadhi ya michezo. Michezo mingi ambayo ilikuwa ikichezwa takribani miaka kumi na tano iliyopita ilibainika kukumbukwaa kwa kiasi kidogo sana. Kwa mijibu wa wazee waliohijiwa katika utafiti huu ni kuwa kuna baadhi ya michezo imepoteza uhalisia na mingine imepotea kabisa.

Mabadiliko ya mfumo wa maisha ambao umewafanya watu kutokuwa na nafasi ya kutosha kukaa na watoto wao kama zamani ni moja ya sababu zilizosababisha kupotea kwa hiyo michezo. Zamani za kale, kulikuwa utamaduni wa wazazi kukaa na watoto wao na kuwafundisha mambo mbalimbali ikiwemo michezo, masimulizi na mafunzo mema. Tabia hiyo kwa sasa inakosekana kwa sababu ya mabadiliko ya usasa katika

jamii mbalimbali. Maendeleo ya sayansi na teknolojia nayo yanachukuwa nafasi katika kuwakosesha watoto na wazazi wao kushughulikia na masimulizi kama hayo na suala hili limesababisha uozo wa maadili wa watoto. Siku hizi watoto wamejikita katika mambo ya kimagharibi yanayobeba mambo uasherati na tabia nyingine ambazo ni mbaya katika jamii. Muda mwingi wa watoto humalizia katika kuangalia runinga na matumizi ya simu, vitu ambavyo huwazuia kushughulikia utazamaji wa michezo ya kuigiza.

Mapendekezo

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti yalivyojitokeza, jamii inavyoweza kufaidika na michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors* kama vile: *Omuntu w'ishokye*, *Akamigano ka rukundo*, *Buri Mbuzi aha nkondo yayo*, *Orweshigishire na Kamuhagama* na watoto wanavyoweza kujengeka kiakili, kimtazamo, mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo:

Mtafiti aligundua kuwa, michezo ya kuigiza haifundishwi katika mtaala wa shule ama za msingi au za sekondari. Kuna haja kwa Wizara ya Elimu kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa michezo ya kuigiza inaingizwa katika mitaala ya shule msingi na sekondari lengo la kuihifadhi malezi bora ya watoto. Hali hii itasaidia kuitunza na kuiendeleza michezo hii ili kuinusuru isipotee kama ilivyobainika. Hii inatokana na ukweli kuwa michezo mingi ya kuigiza malezi ya watoto imeanza kutoweka. Kuna mtazamo kuwa mabadiliko ya kiulimwengu yanaifanya michezo ya kuigiza kutokuwa na uhai wake kamili. Kwa hivyo, ikiingizwa katika mitaala ya shule itasaidia kuhuwisha uhai wake.

Aidha, mtafiti aligundua kuwa katika jamii, hakuna mahali teule ambapo watoto waweza kukaa pamoja kutazama michezo ya kuigiza. Kila mtoto huitazama kivyake na hakuna anayejukumu la kumchagulia mchezo gani wa kutazama kulingana na kiwango

chake. Viongozi wa kisiasa na wa kijamii, kwa kushirikiana na wanajamii, wanapaswa kuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa kunakuwa na ujenzi mzuri utakao toa nafasi kwa watoto kupata maeneo ya kutazama michezo hii ya kuigiza. Utafiti uligundua kuwa ujenzi unaoendelea siku hadi siku unachukuwa nafasi ambayo ilitumiwa na watoto hapo kabla. Ujenzi huo hauzingatii mahitaji ya watoto katika utazamaji wa michezo ya kuigiza. Hali hii huwapa watoto tabu ya michezo kwa kushiriki watoto kidogo, wenye uwezo na wengine kubaki kama wamenyimwa, jambo ambalo haliwafurahishi. Kwa kawaida watoto hupenda wote wawe ni washiriki wa utazamaji wa michezo na hawapendelei kunyimwa haki hiyo.

Mtafiti anapendekeza kufanywa kwa tafiti zaidi kwenye tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zinazohusu malezi ya watoto. Pia mtafiti wa kazi hii alijaribu kuchunguza mchango chanya wa michezo ya kuigiza ya *Kigezi Universal Actors*, kwa hiyo watafiti wa baadaye waweza kutafiti juu ya athari za michezo ya kuigiza kwa malezi ya watoto hasa kwa kujikita katika upande wa athari hasi.

Pia, watafiti wa badaye waweza kufanya tafiti nyingine juu ya malezi ya watoto kwa kuzingatia tanzu mbalimbali za kifasihi kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Mapendekezo ya utafiti huu yanatarajiwa kupunguza au kuondoa kabisa mapungufu yaliyopo. Aidha utekelezaji wake utasukuma maendeleo ya fasihi simulizi kwa ujumla na kuinua hadhi ya fasihi simulizi kwa jamii. Vilevile utafiti huu utatoa mchango mkubwa kwenye taaluma ya fasihi simulizi kwa kuiongezea haiba na hadhi yake stahiki.

MAREJELEO

Akuoko, D.A (2004) *Childrens Folk Games in Ghana*. Katika tovuti <http://www.estcompro/=cfg/ghana.html.pdf>. 10/01/2015

BAKIZA (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press, East Africa Ltd Nairobi, Kenya.

Bakize L. H. (2014), *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*, Moccony Printing Press, Dar - es - Salaam

Beja S. K (2008), *"The Importance of Theory in Social Sciences Research"*. Haijachapishwa

Bulane, M (1981) *"Fasihi Simulizi katika Afrika Kusini, Fasihi Simulizi ya Wenyeji"*. Katika Makala za Semina za Fasihi Simulizi. Dar-es- Salaam, TUKI.

Enon, J. (1998), *Educational Research, Statistic and Measurement*, Department of Distance Education, Kampala.

Eiser, J.R. (1986). *Social Psychology*, Cambridge, Cambridge University Press.

Finnegan, R (1994). *Oral Literature in Africa*, Oxford University Press, Nairobi, Kenya.

Haji, A. A (2006) *Vipera vya Fasihi Simulizi*, Zanzibar, Central Printing Services.

Hardy, M. na wenzake (1995). *Studying Child Psychology*, London, Oxford University Press.

Iona na Opie P. (1969). *Children's Games in Street and Playground*. London, Oxford University Press.

Jones, T.P. (1972). *Creative Learning in Perspective*, London. Oxford University Press.

Khamis.A (2007). *"Utamaduni wa Kiswahili ulivyorithisha na kudumisha amani kwa watoto na vijana wa Zanzibar na taathira za utandawazi"*. Makala Iliyowasilishwa Kwenye Kongamano la Tamasha la Nchi za Jahazi.

King'ei, K.&Kisovi, C.N.M (2005) *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi,Kenya Literature Bureau.

Kothari, C.R (2004), *Research Methodology Methods and Techniques*. Delhi, New Age International Publisher.

Lihamba, A (1981), “*Utendaji katika Sanaa za Maonyesho*”. Katika makala za Fasihi Simulizi, Dar-es-salaam, TUKI.

Masebo, J.A & Nyangwine, N (2002). *Nadharia ya Fasihi*, Kiswahili2, Dar-es-Salaam, Afroplus Industries Ltd

Mbarouk A. A (1981) *Nyimbo za Michezo ya Watoto Katika TAKILUKI*. Fasihi simulizi Zanzibar. Tanzania Publishing House. Dar es Salaam.

Mbarouk, A. A (1994), TAKILUKI, *Nyimbo za Watoto*, Dar-es-Salam, Tanzania Printing House.

Mdowe, S. R (2005) “*Maudhui ya Nyimbo za Watoto Katika Jamii ya Unguja*”, Tasnifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Ndowe (2011), “*Nyimbo za Michezo ya Watoto Zinavyobadilika na Wakati Kifani na Kimaudhui Katika Wilaya ya Magharibi Unguja*”, Shahada ya Uzamili ya sayansi jamii katika fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mohamed, S. A (1990) *Kivuli Kinaishi*, Oxford University Press, Nairobi, Kenya.

Mulokozi, M. M (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M.M & Mung'ong'o (1993). “*Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*” Katika makala za semina ya umoja wa waandishi wa vitabu Tanzania, Dar-es- salaam.

Mbaga, N.O (1981) “*Chimbuko la Sanaa za Maonyesho*”. Katika makala za Fasihi Simulizi, Dar-es-Salaam, TUKI.

Nguro, A (2003) *Fasihi Simulizi*. Phoenix Publishers Ltd Nairobi..

Nguro, A. (2005), *Fasihi Simulizi*, kwa Shule za Sekondari, Phoenix Publisher Ltd, Nairobi, Kenya.

Njogu, K. & Chimerah, R (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*; Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K & wenzake (2006). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*, Nairobi, Twaweza Communications.

Ponera A. S (2010) *Ufutuhi Katika Nathari za Shaaban Robert: Maana yake, Sababu za Kutumiwa na Athari zake kwa Wasomaji*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma. Haijachapishwa.

Rotich, A. K (2008) “*Nyimbo za Watoto za Shule za Chekechea na za Msingi katika Manispaa ya Bomet; Uchunguzi wa Kiuamilifu*” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Falsafa ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Ruhumbika, G. (1983) “*Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili*”, Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III, Fasihi, Dar-es- Salaam, TUKI

Said A. M (2005) *Maana na Mafunzo Yanayopatikana Katika Nyimbo za Michezo ya Watoto Wadogo, Unguja*, Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kiislam Uganda. (Haijachapishwa).

Senkoro, F.E.M.K (1982) *Fasihi na Jamii*, Dar-es- Salaam. Press and Publishing Centre.

Senkoro, F.E.M.K (2011) *Fasihi*, KAUTTU, Dar es Salaam.

Shamsi, R. M. (1994). *Nyimbo na Michezo ya Watoto Wadogo*, Moshi, Nyota Publishers Ltd.

Shamoun, H.A (1992) “*The Use of Theatrical Forms and Games for Children Mental and Physical Growth*”, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam. (Haijachapishwa)

Shima G. (2012) *Nafasi ya Vielelezo Katika Fasihi ya Watoto*, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Songoyi, E. M (1997) *Oral Literature*, The Open University of Tanzania.

TUKI, (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, Nairobi, Kenya.

Ussi, H. M (2010) “*Dhima ya Michezo ya Watoto ya Kuigiza ya Kigezi Universal Actors katika kujamiisha watoto wa jamii ya Wamakunduchi*” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kiislam Uganda. (Haijachapishwa).

Wallace, R. A & Wolf (1987) *Contemporary Sociologic Theory*, New York, Prentice Hall Publishers.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasih, Istilahi na Nadharia*. Nairobi, Focus Publishers Ltd.